**P320/2**
**KISWAHILI**
**Paper 2**
**July 2019**
3 Hours

# ACEITEKA MOCK EXAMINATIONS 2019

## Uganda Advanced Certificate of Education

FASIHI YA KISWAHILI P320/2

**Karatasi ya Pili**

MUDA: Saa Tatu

**MAAGIZO:**

a) *Jibu maswali **matatu tu**.*
b) *Chagua swali moja kutoka sehemu ya **A, B, CH** au **D.***
c) ***Sehemu B ni ya lazima kwa wanafunzi wote. Chagua swali moja katika sehemu hii.***
d) *Usijibu swali zaidi ya moja kutoka kitabu Kimoja wala maswali mawili kutoka sehemu moja.*
e) *Nadhifisha mwandiko wako.*

Ecolebooks.com

# SEHEMU A

**Juliasi Kaizari:** William Shakespeare.

1. a) Ni kweli kwamba Mungu huongea na watu wake kwa njia maalum. *Thibitisha ukweli wa kauli hiyo* ukirejelea ushahidi kutoka *tamthilia ya Juliasi Kaizari.* *(Alama 16)*

   b). Mauti ya Juliasi Kaizari huko Roma yalisababishwa na masuala gani? Eleza kwa mujibu wa tamthilia hii. *(Alama 17)*

2. a) Tamaa ya uongozi ni chanzo cha migogoro iliyosababisha maafa yanayokithiri katika jamii ya William Shakespeare. Jadili kwa mujibu wa *tamthilia ya Juliasi Kaizari.* *(Alama 17)*

   b). Vijana kama wanavyoitwa viongozi wa kesho, wanapata maadili gani baada ya kuisoma *tamthilia ya Juliasi Kaizari*? Eleza. *(Alama 16)*

**Mzalendo Kimathi:** Ngugi wa Thiong'o na Micere Mugo.

3. a) Uzalendo ni ile hali ya mwananchi kuipenda nchi yake kwa dhati na kujitolea kuipigania katika kila hali. Ukirejelea jamii ya Ngugi wa Thiong'o, eleza jinsi uzalendo unavyojitokeza. *(Alama 20)*

   b) 'Amani haiji ila kwa ncha ya upanga'. Tathimini ukweli wa msemo huo ukirejelea tamthilia ya Mzalendo Kimathi. *(Alama 13)*

4. a) Jadili mandhari ya hadithi ya Mzalendo Kimathi. *(Alama 18)*

   b) Tamthilia ya Mzalendo Kimathi ina umuhimu gani kwa jamii ya kisasa? Fafanua. *(Alama 15)*

# SEHEMU B

**Janga la Werevu:** Said A. Mohamed

5. *Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yaliyo hapo chini.* *(Alama 34)*

**Bamkuu**: Hayo si hapa petu lakini……...

**Busara**: Hayo hatuyajui wala hatuna hakika nayo. Na kama wasemavyo watu lisemwalo lipo Kama halipo laja. Tuna vizuizi gani vya kuzuia hayo katika kinyanganyiro cha Pesa na ufisadi uliojaa?

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

*(kimya. halafu……Ghafla anaingia Kristy, msichana aliye chuo kikuu pia mwaka Wa kwanza. Yeye ni binti wa nyumba hii lakini tofauti na busara, ana hamaki za Ndani kwa ndani zinazomla na kummaliza. Anaingia Kristy nyumbani kutoka Chuoni.)*

**Kristy**: Baba, baba, mama, mama, huu sasa ni mwezi wa sita maji hayapatikani chuoni kwetu- yamekatika moja kwa moja. Yameyoyoma kabisa kabisa. Hayatoki tena mabombani. Mjadala wetu chuoni unaelezea kuwa vianzo vya maji vimekauka. Na kisha tunatabiri kwamba litazuka balaa la watu kugombana na kupigana vita kwa nia ya kuhodhi peke yao maji ya taifa zima. Ati kweli? Mnaonaje nyinyi? Mnaonaje mkapunguza uharibifu wa maji na kuacha kuitumia misitu kwa maslahi yenu utu ya kibiashara?

**Bimkuu:** Walimu wenu wanakufundisheni mambo yasiyo na msingi, Mambo maovu kabisa.

**Kristy:** Lakini hata kwenye redio kila siku habari za ukame tunazisikia.
Na hata katika runinga tunajionea. Ama ni ukame
Na watu, mimea na wanyama wanaoangamia kwa njaa na kiu,
Au mafuriko yanayofunika roho za watu na kila kitu chao. Au
Jinsi dunia inavyoharibiwa kwa moshi wa magari na madawa.
Viwanda vinamwaga sumu mitoni, meli zinatumbukiza
takataka baharini. *Vadau* vinatumiwa na wakubwa kumwaga
uchafu maziwani. Kila kiumbe kinalia maji, maji safi.
Rasilimali ya maji imeleta cheche za moto duniani kote. Si
Mashariki ya kati si uajemi si Afrika si Ulaya. *(kwa bezo)* eti
Tunapalilia maendeleo!

**Mswali:**

**(**a) Liweke dondo hili katika mkutadha wake. *(Alama 08)*

**(**b) Kulingana na dondoo hili, Kristy na Bimkuu wanatofautianaje kimtazamo. *(Alama 04)*

(ch) Tambua mbinu za kisanaa zinazopatikana katika dondoo hili. *(Alama 08)*

(d) Ni uharibifu wa aina gani wa mazingira ambao Kristy anazungumzia katika dondo? *(Alama 04)*

(e) Ni ujumbe gani unaojitokeza katika dondoo hili? *(Alama 06)*

(f) Ukirejelea dondoo hili, eleza madhara yanayosababishwa na uharibifu wa mazingira, *(Alama 04)*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

## ARI KATINI MWACHOFI: *Mama ee*

6. *Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yaliyo hapo chini.* *(Alama 34)*

**TENGE:** Ukinisamehe wewe sitajali ya walimwengu mama!

Umenisamehe mama? Mama! Mama! Kosa la mara moja tu….

*(Aingia baba – ghafla amshika Tenge na kumcharaza fimbo tatu kabla mkewe hajamzuia kwa kushika fimbo).*

**BABA:** *(Kwa mabezo na kuiga.)* "Kosa la mara moja". Nisikuone nyumbani kwangu tena. *(Tenge alia Zaidi.)* Toweka kabisa mbele ya macho yangu na usiniite tena baba. "Kosa la mara moja"! Kwani hukujua mwisho wake? Huyo mamako hakuwaambia? Kila siku "George amekuja, George amekuja". Kumbe ndiyo hayo. Umepata natija sasa! George yuko shuleni! Wewe je? Umeambulia patupu. *(Anataka kuchukua fimbo kumchapa lakini mkewe amzuia. Aendelea kusema kwa ghadhabu.)* ondoa aibu hii kijijini kwangu. Pesa zangu zote za darasa la kwanza hadi sasa nazitaka, sijali utapata vipi hata kama ni kwa kuongeza uhawara. *(Akimgeukia mkewe na kumsukuma).* Na wewe walilia nini? Hivi ndivyo unavyowalea wasichana wako? *(Ataka kumchapa fimbo lakini Tenge aingia kati na apigwa yeye. Aanguka chini azidi kupigwa. Mama apiga yowe.)* Mama uui! Mama uui! *(Atokea kakake Tenge. Ajaribu kumzuia babake lakini asukumwa.)*

**KAKA:** Ebu – Baba ebu. Kuna nini? Wacha vita baba.

**BABA:** Wacha nimfundishe Malaya huyu apate kurejesha pesa zangu zote nilizopoteza ati karo ya shule, kumbe ni karo ya kujifunza umalaya.

**Maswali:**

a) Liweke dondoo hili katika mkutadha wake. *(Alama 08)*

b) Ni ujumbe gani unaojitokeza katika dondoo? Fafanua ukitoa mifano. *(Alama 08)*

c) Eleza mbinu za kisanaa zilizotumiwa katika dondoo hili. *(Alama 08)*

d) Tambua chanzo cha mgogoro katika dondoo hili. *(Alama 04)*

e) Eleza mafunzo matatu yanayopatikana katika dondoo hili. *(Alama 06)*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Ecolebooks.com

## SEHEMU CH

**Kivuli Kinaishi:** Said A. Mohamed

7. a) "Giningi ni mfano wa jamii yenye uongozi wa kidikteta", thibitisha uyakinifu wa kauli hiyo kwa kurejelea ushahidi kitabuni. *(Alama 16)*

   b) Ukirejelea mifano kadhaa kwenye tamthilia ya Kivuli Kinaishi,eleza jinsi wanaginingi walivyojitahidi kutetea utu na haki zao. *(Alama 17)*

8. a) Dhana ya Kivuli kinaishi imepewaje kipaumbele katika jamii ya *Kivuli Kinaishi*? Fafanua huku ukitoa mifano kadhaa. *(Alama 18)*

   b) Kwa mujibu wa Tamthilia ya Kivuli Kinaishi, eleza jinsi mwandishi alivyofanikiwa kumchorea msomaji picha halisi ya ukatili uliokithiri katika jamii. *(Alama 15)*

**JOHN RUGANDA:** Mizigo

9. (a) Eleza shughuli au majukumu yaliyogeuka kuwa mizigo kwa mhusika Tinka ukirejelea yaliyomo katika tamthilia ya Mizigo. *(Alama 17)*

   (b) Jadili mambo yaliyochangia pakubwa katika kusambaratika kwa familia ya wamala. *(Alama 16)*

10. (a) Kwa kutoa mifano jadili mbinu za kisanaa zilizotumiwa na Ruganda katika tamthilia ya Mizigo. *(Alama 18)*

    (b) Jadili maudhui yanayojitokeza katika tamthilia ya Mizigo. *(Alama 15)*

## SEHEMU D

**EBRAHIM HUSSEIN:** Kwenye Ukingo wa Thim

11. a) Eleza masuala nyeti katika tamthilia hii Kwenye Ukingo wa Thim. Jadili. *(Alama 17)*

    (b) Eleza umuhimu wa mhusika Martha katika ujenzi wa tamthilia ya Kwenye Ukingo wa Thim. *(Alama 16)*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

12. a) Eleza aina kadhaa za migogoro inavyojitokeza katika tamthilia ya Kwenye Ukingo wa Thim. *(Alama 17)*

(b) Vijana wa kisasa wanaweza kujifunza mambo yapi kutokana na matukio yaliyomo katika tamthilia ya Kwenye Ukingo wa thim? *(Alama 16)*

**Zabibu Chungu:** Boukheit Amana

13. a) Tamthilia ya Zabibu chungu imebeba maadili yepi kwa vijana wa kizazi kipya? Fafanua. *(Alama 20)*

b) Mwandishi akipitia wahusika kadhaa ameonyeshaje tofauti kati ya mahitaji ya mila na maisha katika dunia ya kisasa? Fafanua ukirejelea tamthilia nzima. *(Alama 13)*

14. a) Zabibu chungu ni tamthilia inayorejelea maisha halisi katika jamii zetu za kiafrika. Thibitisha ukweli wa kauli hiyo ukirejelea mifano kitabuni. *(Alama 17)*

b) Vijana wa kisasa wanaotaka kuingilia suala la ndoa wanafaa kuzingatia misingi yepi ya kujengea ndoa imara? Fafanua. *(Alama 16)*

***TAMATI***

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM